KANISA LA WAADVENTISTA WA SABATO UNIONI YA KUSINI MWA TANZANIA

CHAMA CHA WACHUNGAJI/HUDUMA ZA MAOMBI

SIKU 100 ZA MAOMBI: MACHI 27 – JULAI 04, 2020

MADA: KUMWITA YESU KATIKA HITAJI LETU LA HARAKA

Limeandaliwa na: Ron Clouzet - Ministerial Secretary of the Northern Asia-Pacific Division

Mtafsiri: Mch. Herbert I. Nziku – Mratibu - Huduma za Maombi: STUM

JUMA LA SABA, MEI 8 – 14, 2020

BORA KULIKO TUWEZAVYO KUWA NAVYO

Mwaka 2001, ilikuwa karibu nife. Daktari wa dharura alisema kuwa yumkini nilikuwa nimebakia na masaa matatu ili nife. Nilipata aina fulani ya malaria nilipokuwa nafanya kazi ya uinjilisti pamoja na wanafunzi wenzangu kule Afrika ya Magharibi, na dalili zilianza kuonekana tu niliporudi Marekani. Nilikuwa na homa kali sana, maji yaliisha mwilini, na nilipata maumivu makali ya kichwa. Nilijihisi mgonjwa na nilifikiri kuwa ningetoweka na kufa dakika yo yote. Dalili zilipojitokeza nilikuwa kwenye majukumu ya kanisa. Nilidamka na mapema uwanja wa ndege ili kuwahi ndege ya kurudi, nilipenda homa ingenipata nikiwa nyumbani.

Mke wangu alinikimbiza kwenye chumba cha dharura hospitalini. Wakati huo nilikuwa na maluweluwe, na sikuweza kumeza maji pasipo kutapika. Nilipoteza fahamu muda mfupi baada ya kupelekwa chumba cha wagonjwa mahututi kwa njia ya kiti cha wagonjwa. Fahamu zilinirudia tena, ninakumbuka maisha yalikuwa kama yako kwenye mwendo wa pole pole. Kila dakika ilionekana kama saa moja na kila saa kama kama siku moja. Ninakummbuka mke wangu, Lisa, alinileta watoto wetu, wakati ule walikuwa na umri wa miaka 14, 12, na 10 tu, na nilipowaona nilianza kulia kimya kimya. Ninakumbuka wauguzi na wengine walikuwa wakinichunguza kwa lengo tu la kumwangalia mgonjwa wa malaria, maana ugonjwa huo ni nadra sana kule Marekani.

Ilikuwa wazi kwamba nilikuwa nakufa. Baadaye nilielewa kuwa aina ile ya malaria ndio mbaya zaidi. Ilikuwa na uwezekano mkubwa wa kukuua, ingawa, ukipona, hungekuwa na dalili za kuirudia, labda uugue tena. Watu wengi walianza kuomba. Mke wangu aliomba na watoto wangu waliomba. Wazazi wangu na wanafamilia wengine waliomba. Wenzetu kule Southern Adventist, nilikokuwa nafundisha waliomba. Rafiki zangu toka sehemu nyingi duniani waliomba. Na idadi ya wachungaji isiyohesabika katika nchi nzima waliomba. Nilipiga hesabu yumkini watu 2,000 walikuwa wkiniombea katika siku zile.

Kupona haingekuwa rahisi. Dawa inayofaa haikuwepo. Rafiki zangu ambao ni madaktari walianza kuwashinikiza madaktari wa hispitali ile kufanya haraka kabla hawajachelewa. Hatimaye ikapatikana dawa iitwayo kwinini kutoka jimbo la Atlanta, na waliweza kupata kiasi fulani tu. Kwinini ni dawa ya zamani iliyotumika kutibu malaria na baadhi ya magonjwa mengine hatari, lakini leo inatumika kwa nadra sana. Ni dawa yenye sumu kiasi na inaweza kuleta madhara makubwa baada ya kuitumia. Lakini itaponyesha malaria. Saa arobaini na nane baada ya kulazwa hospitalini, nilipewa kwinini, lakini haikuonesha muujiza uliotarajiwa. Siku moja baadaye, siku ya Sabato, nilikuwa mgonjwa kama nilivyokuwa kabla ya hapo.

Katika hali yangu ya udhaifu na ugonjwa nilisali pia. Lakini sala yangu ilikuwa ni shukrani zaidi kuliko kuomba. Nilikuwa nimeyatoa maisha yangu kwenye mikono ya Mungu na nilikuwa tayari kusema kwa heri iwapo ingekuwa ni zamu yangu kwenda. Jambo pekee nililojutia, ambalo pia nililiombea, lilikuwa ni kumwacha mke wangu na watoto watatu, na kuwaacha watoto bila baba. Lakini hilo pia lilikuwa mikononi mwa Mungu. Nilikuwa na amani kwamba yote yangekuwa

sawa. Siku ya Sabato mchana, wenzangu kadhaa toka Chuo Kikuu na mchungaji wangu wa kanisa walikuja. Walinifanyia huduma ya kupaka mafuta na kuniombea tena, kwa mujibu wa Maandiko (Yakobo 5:13-15). Usiku ule, Lisa alikaa na mimi usiku mzima. Alihofia hakika kwamba ilikuwa ndio siku yangu ya mwisho. Mnamo ya 11 alfajiri, asubuhi iliyofuata, mwunguzi alikuja ili kuchukua damu, kama walivyokuwa wakifanya kila asubuhi. Masaa manne baadaye, daktari bingwa alikuja chumbani kwangu. Kwa mara ya kwanza nilikuwa tayari kukaa. Aliniambia kwamba hawakuweza kupata hata chembe ya malaria kwenye mfumo wa mwili wangu. Kiasi fulani yalikwamyameondoka yote. Alionesha mshangao kwa kuwa dawa ilikuwa imefanya kazi kwa haraka sana. Lakini nilijua kulikuwa na sababu nyingine iliyofanya niwe huru dhidi ya malaria. Ilikuwa ni maombi ya wapendwa wangu na maombi ya watakatifu. Ninaamini kuwa Mungu alikubali kuniponya kwa rehema zake, kwa sababu tu watu wake walimwomba aniponye.

"Mwokozi yule yule mwenye huruma yupo hai leo, na yupo tayari kusikiliza maombi ya imani kama alivyoonekana akitembea miongoni mwa watu...Ni sehemu ya mpango wa Mungu kutupatia sisi, kwa kujibu maombi ya imani, kile ambacho hangeweza kutupatia tusingeomba." (GC, p. 525). Yesu hakupaswa kuniponga. Alikuwa hahitaji cho chote toka kwangu. Nilihitaji kila kitu toka kwake, na bado nahitaji. Lakini, hata hivyo alitenda.

Sio kila jambo linalotishia maisha humalizika kwa namna moja. Lakini, haijalishi Mungu mponyaji ni yule yule. Yeye ni wa kutumainiwa. Inapasa ashukuriwe kwa namna zote, kwani hakuna namna kwamba atajibu maombi yetu kwa njia itakayokuwa na madhara kwenye roho zetu. Cho chote tunachopokea toka kwake ndicho bora kuliko vyote tuwezavyo kuwa navyo.

Maswali ya Moyoni: Je! Unaamini kwamba Mungu anaweza kuponya magonjwa ya aina zote, yakijumuisha kwa umuhimu zaidi gonjwa la kuambukiza la dhambi? Je! Leo maisha yako yapo sawa mbele za Mungu? Una amani pamoja naye muda huu?

Changamoto Hai ya Moyoni: Ugonjwa ni sehemu ya ulimwengu huu uliovunjika. Hakuna aliye salama dhidi ya ugonjwa, lakini tunao uchaguzi namna ya kukabiliana nao. Wakati wa mahitaji ya haraka tunaweza kumng'ang'ania Yesu, tukiomba kwa ajili ya mahitaji ya kiroho na ya kimwili, na tunaweza kupumzika tukiwa tumehakikishiwa, bila kujalisha matokeo ugonjwa yatakuwaje, kwamba kwa vile tunamtazama yeye, tunaweza kuwa salama. Kuwa na imani imara wakati wa ugonjwa huanza kwa kufanyia mazoezi imani wakati wa afya njema. Je! Unachagua kumwamini leo? Upo tayari kukubali, hata kifo, ukijua kuwa hatimaye, magonjwa yote yataponywa ile asubuhi ya ufufufo kwa wale wanao mwamini?

"Bwana wetu Yesu Kristo alikuja ulimwenguni hapa kama mtumishi asiyechoka wa mahitaji ya wanadamu, 'aliutwaa udhaifu wetu, Na kuyachukua magonjwa yetu' ili aweze kuhudimia kila hitaji la wanadamu. Alikuja kuondoa mzigo wa ugonjwa na unyonge na dhambi. Ilikuwa ni utume wake kuwaletea watu urejeshaji kamili; Alikuja kuwapatia afya na amani na ukamilifu wa tabia." (MH, p. 17)

Mapendekezo ya aya za ziada za kusoma juma hili:

- Ellen White, *Ministry of Healing*, chapter 16, "Prayer for the Sick"
- Ron Clouzet, *Adventism's Greatest Need: The Outpouring of the Holy Spirit*

Siku ya 43, Ijumaa, Mei 8, 2020

Taarifa ya Sifa

- Brittney na Vanessa, B., wanasema, *"Kanisa letu lilianza kukutana kila usiku ili kuomba kwa njia ya mtandao. Hili limemleta kila mmoja karibu na mwenzake kwani tunaonana kila siku. Hii ni baraka!"*
- Mico, F., anasema, *"Hii hali imetufanya tutambue kuwa kanisa sio jengo, ni watu!"*

MAMBO YA KUOMBEA

- Ombea makanisa yaliyopoteza washiriki kwa sababu ya COVID -19.
- Ombea washiriki wanaopambana na masuala mbali mbali ya kiafya kama vile saratani, magonjwa ya upungufu wa kinga, huzuni, na masuala mengine.
- Ombea waliokuwa Waadventista wakaliacha kanisa. Ombea watu walio kwenye maeneo ya ushawishi wao ambao yawezekana wameongozwa kwenda mbali na Mungu kwa sababu ya kurudi nyuma kwao.
- Ombea washiriki wapya waliojiunga na kanisa kupitia mikutano mbali mbali ya TMI katika miaka iliyopita.

Siku ya 44, Jumamosi, Mei 9, 2020

KUMJUA YESU

"Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma" (Yohana 17:3)

"Kristo alikuja kumdhihirisha Mungu kwa ulimwengu kama Mungu wa upendo, mwingi wa rehema, upole, na huruma. Giza nene ambalo kwalo Shetani alijitahidi kukigubika kiti cha enzi ya Uungu lilifagiliwa mbali na Mwokozi wa ulimwengu, na Baba akaoneshwa wazi kwa watu kama nuru ya uzima." (5T 738)

Maswali ya Moyoni: Uzima wa milele sio tu kuishi milele, bali uzima wa milele ni kuendeleza kina cha uhusiano wa upendo pamoja na Mungu. Je! Unajua zaidi ukweli kumhusu Yesu, au umamjua yeye binafsi kama Mwokozi na Rafiki? Kwa nini usianze umilele leo kwa kumwomba Yesu ajidhihirishe mwenyewe kwako kwa kiwango cha kina, unapotumia muda katika maombi, kujifunza Biblia na kuwashirikisha wengine upendo na ukweli wake?

Taarifa ya Sifa:

- Thierry, T., anasema, *"Ninawashirikisha rafiki zangu 90 'Siku 100 za Maombi.' Pia niliweza kugawa kitabu cha 'Pambano Kuu' kwa watu wengi niliokuwa na mawasiliano nao. Mtu mmoja asiye Mwadventista aliniomba tujifunze pamoja unabii wa Danieli na ufunuo."*
- Gloria, D., anasema, *"Mungu ametubariki kwa kuwa na uwezo wa kuendesha programu yetu ya kusambaza chakula bila kujali janga hili."*

MAMBO YA KUOMBEA

- Ombea washiriki ulimwenguni kote wanaoanzisha au kuendesha vituo vya mvuto viitwavyo Life Hope Centers of Influence.
- Ombea watu wa visiwa vya Fiji na Vaniatu ambao wameathirika kwa kimbunga cha hivi karibuni.
- Ombea taasisi zetu za elimu kote ulimwenguni. Ombea waweze kuwa na uwezo wa kutafuta njia za kutoa elimu ya Kikristo kwa njia ya mtandao na njia zingine. Omba kwamba ziwe tayari kuendelea kuwa na mvuto chanya wa kiroho kwa wanafunzi, na ziendelee kuwa imara kifedha.

Siku ya 45, Jumapili, Mei 10, 2020

HUDUMA YA YESU

"Basi, iwapo tunaye kuhani mkuu aliyeingia katika mbingu, Yesu, Mwana wa Mungu, na tuyashike sana maungamo yetu. Kwa kuwa hamna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi. Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji." (Waebrania 4:14-16)

"Mwana wa Mungu... ametimiza ahadi, na amekwenda mbinguni, kuchukua serikali ya jeshi la mbinguni. Alikamilisha awamu moja ya ukuhani wake kwa kufa msalabani kwa ajili ya taifa lililoanguka. Sasa anakamilisha awamu nyingine kwa kuomboleza mbele za Baba juu ya kesi ya mwenye dhambi anayetubu, akiwasilisha kwa Mungu sadaka za watu wake. Kwa kuchukua asili ya wanadamu, na katika asili hii akashinda vishawishi vya adui, na kwa kuwa na ukamilifu wa kiungu, amepewa hukumu ya ulimwengu. Kesi ya kila mmoja italetwa ili kupitiwa mbele zake. Atatamka hukumu, akimpatia kila mtu kwa kadiri ya kazi zake." (Manuscript 42, 1901)

Maswali ya Moyoni: Yesu alifanyika mwanadamu, akafa, akafufuka, na sasa hivi anasimama katika hekalu la mbinguni kama mwakilishi wa wote waliosalimisha maisha yao kwake. Unapoomba, anasikiliza. Unapotafuta msamaha wa dhambi, na ushindi, anakusikia na mara moja atakupatia nguvu inayohitajika kushinda. Tunapoishi katika nuru ya hukumu, Je! Umemfanya Yesu, Kuhani Mkuu mwenye huruma, kuwa wakili wako (1Yohana 2:1)? Je! Umetafuta kimbilio katika haki yake? Je! Utamruhusu sio tu kukufunika kwa haki yake, bali pia kukujaza haki yake kwa kutenda kazi alizokuandalia (Waefeso 2:10)?

Taarifa ya Sifa:

- Sheri, M., ansema, *"Ninamshukuru Mungu! 'Siku 100 za Maombi' zimeimarisha imani yangu katika wakati huu mgumu."*
- Rose, S., anasema, *"Kwa sababu ya hili janga kundi letu liitwalo, 'Power of Prayer Chat Group' (yaani, Kundi la Nguvu ya Maombi kwa njia ya mtandao) limekuwa hai zaidi kwani tunapata muda wa kuomba pamoja karibu mara 5-6 kila siku."*

MAMBO YA KUOMBEA

- Ombea watu wasio na makazi katika maeneo yote ulimwenguni ambao wanategemea umati mkubwa wa watu kwa ajili ya msaada na sasa wamo kwenye uhitaji mkubwa kwa sababu ya mazuio.
- Ombea washiriki wazee wasio na uwezo wa kuungana na familia zao wakati wa hii zahama. Ombea wale wanaopambana na magonjwa ya akili na wamechanganyikiwa sana wakati huu.
- Ombea ndoa ambazo kwa sasa zipo kwenye shinikizo la ziada. Ombea wanandoa wanaopambana wapate uponyaji, msaada, na unyenyekevu wanampomtazama yesu.

Siku ya 46, Jumatatu, Mei 11, 2020

UPENDO WA YESU

"Kama vile Baba alivyonipenda mimi, nami nilivyowapenda ninyi, kaeni katika pendo langu." (Yohana 15:9)

"Kama nitaokolewa katika ufalme wa Mungu, daima nitadumu katika kutambua vina vipya katika mpango wa Mungu wa wokovu. Watakatifu wote waliokombolewa wataona na kufahamu, kuliko ilivyokuwa kabla ya hapo, upendo wa baba na Mwana, na nyimbo za sifa zitaripuka toka kwenye ndimi za watu wenye hali ya kutokufa. Anatupenda, aliutoa uhai wake kwa ajili yetu. Tutaimba utajiri wa upendo wenye kuokoa, tukiwa na miili yenye utukufu, uwezo uliokuzwa, mioyo iliyotakaswa, na midomo isiyo na unajisi." (Letter 27, 1890)

Maswali ya Moyoni: Mungu ni upendo. Yeye ndiye mwanzilishi wa upendo. Hakuna upendo ulio safi zaidi ya upendo ulio ndani ya Mungu. Ikiwa Yesu anatupenda kama Baba anavyompenda Yesu, kutakuwa na nini cha kuvutia zaidi ya kuwa pamoja na yeye katika upatanifu kamili? Upendo wa Yesu hauna kifani! Je! Kuna mambo yanayoendelea maishani mwako unayoyapenda zaidi ya Yesu? Kuna jambo fulani lililovutia mapenzi ya moyo wako? Mwombe Yesu akuguse kwa upendo kamili anaotumia kukupenda. Kwa nini usichague leo kuukubali upendo huu ndani ya moyo wako na kuufanya kuwa kichocheo kikuu kwa ajili ya safari yako ya imani?

Taarifa ya Sifa:

- Katika baadhi ya nchi na majimbo ya Marekani wameanza kufungua biashara (kwa masharti)
- Idadi ya wagonjwa na vifo vya COVID-19 angalau imepungua kuliko ilivyotabiriwa kabla.

MAMBO YA KUOMBEA

- Ombea miradi mbali mbali ya ujenzi kama vile makanisa na shule ulimwenguni kote.
- Ombea utoaji endelevu na uaminifu katika kurudisha zaka na sadaka.
- Ombea visiwa vya St. Vincent na Grenadines vinavyokabiliwa na ukame mbaya sana pamoja na janga hili. Ombea wapate mvua, na Mungu abariki utume wa makanisa mahalia.
- Ombea washiriki waliokumbwa na hofu wakati wa hili janga.
- Omba kwa ajili ya utambuzi katika kuelewa tofauti kati ya kutii kanuni za usafi zinazohamasishwa na serikali na ibada ya uwongo inayolazimishwa.

Siku ya 47, Jumanne, Mei 12, 2020

IMANI YA YESU

"Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu." (Ufunuo 14:12)

"Imani katika uwezo wa Kristo kutuokoa kabisa tena kikamilifu in imani ya Yesu" (3SM 172)

Maswali ya Moyoni: Tunaishi katika siku za mwisho. Sasa ni wakati ambapo matumaini kamili katika uwezo wa Mungu wa kutupatia ushindi, yanahitajika zaidi kuliko wakati mwingine! Yesu aliutoa uhai wake, kifo chake, ufufuko, na Neno lake lenye ahadi na maelekezo kwako. Ameahidi kufanya kazi ya kukuokoa. Inashangaza, si ndio? Je! Unatamani kuamini hili kweli kweli na kuukubali ukweli huu pamoja na matokeo yake yanayobadilisha maishani mwako? Je! Unataka Yesu aichukue imani yako ndogo na dhaifu na kuibadilisha kuwa imani isiyotikisika? Kwa nini usimwombe kuifanya kazi hiyo dani yako unapoendelea kufuata mapenzi yake siku kwa siku?

Taarifa ya Sifa: Inatia moyo kusikia namna makanisa yetu mengi, wachungaji, na washiriki wengine wamekuwa wabunifu wakiweka mtandaoni kila mara fursa za ibada, maombi na ushirika kwa ajili ya washiriki wao mahalia.Hii itakuwa ni faida kubwa kwa kanisa kwa kadiri tunavyosonga mbele. Hii inatusababisha kufikiri njia mpya na chanya namna ya kuwafikia watu wanaotuzunguka wanaomhitaji Yesu

MAMBO YA KUOMBEA

- Ombea miradi mbali mbali ya utume na jitihada za uinjilisti kule Kaskazini mwa Saluwesi, nchini Indonesia
- Ombea Waadventista kule Cairo, Misri ambao wanapambana kupata uwezo wa kupokea misaada ya chakula kutoka kwa washiriki kutokana na baadhi ya masharti ya maeneo mahalia.
- Ombea washiriki kule Kaskazini magharibi mwa Nigeria ambao wanauinua ujumbe wa injili bila kujali hatari inayowajia kutoka kwa vikundi vya kigaidi, majambazi na wahalifu ambao wana nguvu sana katika lile eneo.
- Ombea wanafunzi kule Ufilipino wanaokabiliwa na masuala yanayohusiana na kusoma siku ya Sabato kufuatia ratiba mpya iliyotolewa wakati wa janga hili.

Siku ya 48, Jumatano, Mei 13, 2020

UWEPO WA YESU

"Lakini mimi nawaambia iliyo kweli; yawafaa ninyi mimi niondoke, kwa maana mimi nisipoondoka, huyo Msaidizi hatakuja kwenu; bali mimi nikienda zangu, nitampeleka kwenu." (Yohana 16:7)

"...na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari." (Mathayo 28:20)

"Tangu wakati huo, Kristo alikaa daima ndani ya mioyo ya watoto wake kwa njia ya Roho. Muunganiko wao pamoja naye ulikuwa wa karibu zaidi kuliko alipokuwa nao yeye mwenyewe. Nuru, na upendo, na uweza wa Kristo akaaye ndani uliangaza nje kupitia kwao, kiasi kwamba watu, waliowatazama, 'wakastaajabu, wakawatambua ya kwamba walikuwa pamoja na Yesu" Matendo 4:13" (Steps to Christ, p. 74)

Maswali ya Moyoni: Je! Umewahi kutamani kwamba ungekuwa hai wakati Yesu alipokuwepo duniani? Vipi kutembea na kuzungumza naye? Lengo lenye nguvu la injili ni kukupatia wewe kitu fulani kilicho bora zaidi! Yesu anataka kuishi ndani yako, ili akufanye ufanane naye kwa njia ya huduma ibadilishayo ya Roho Mtakatifu. Je! umewahi kumwomba Yesu akubatize kwa Roho Mtakatifu ili kwamba ndani yako uweze kuuhisi na kuuona uwepo wake? Yesu alitwambia tuombe karama ya Roho wake kila siku (Luka 11:13) Kwa nini sasa hivi usimwalike Kristo akae ndani yako kwa njia ya Roho?

Taarifa ya Sifa:

- Kwa sababu ya hili janga, watu wengi wanaotuzunguka wako wazi na wenye kupokea ushuhuda wetu na uelewa na Maandiko. Msifu Mungu kwani wakati wa janga hili anaokoa wengi kwa ajili ya umilele pamoja naye!

MAMBO YA KUOMBEA

- Ombea watu wanaopambana na kukandamizwa na mapepo na kupagawa. Waombee ili wafunguliwe toka katika uwezo wa Shetani. Ombea familia zao, na hasa watoto ambao wazazi wao wameathirika.
- Ombea maelfu ya makundi na makanisa mapya yaliyoanzishwa ulimwenguni kote kwamba yabaki kuwa imara na yenye nguvu bila kujali janga lililopo.
- Ombea wachungaji na viongozi wa kanisa katika nchi zenye huduma mbaya za afya.
- Ombea vituo vya redio za Kiadventista ulimwenguni kote, vinavyowafikia wasioweza kufikiwa kwa njia zingine.

Siku ya 49, Alhamisi, Mei 14, 2020

REHEMA YA YESU

"Bwana ni mwenye neema na haki, Naam, Mungu wetu ni mwenye rehema." (Zaburi 116:5)

"Roho zilizomjia Yesu, katika uwepo wake zilijisikia kuwa hata kwa ajili yao kulikuwa na njia ya kukimbia shimo la dhambi. Mafarisayo walikuwa tu na dharau na hukumu dhidi yao; lakini Kristo aliwasalimia kama watoto wa Mungu, waliotengwa kabisa toka katika nyumba ya Baba, lakini hawajasahauliwa na moyo wa Baba. Na ile shida yao na dhambi iliwafanya kipekee wawe walengwa zaidi wa rehema yake. Kwa kadiri walivyotanga mbali toka kwake, ndivyo ilivyo kuwa hamu yenye bidii na kafara kuu kwa ajili ya kuokolewa kwao." (COL, p. 186)

Maswali ya Moyoni: Neema ya Mungu kwetu ni matokeo ya moja kwa moja ya rehema yake kuu kwa wale wanaoteseka chini ya dhambi na matokeo yake. Unapotambua rehema yake kwako, kama ilivyodhihirishwa katika Yesu, ni kitu gani kinachokuzuia usije kwake leo, kama ulivyo, na kuzisalimisha kwake kona za giza za maisha yako? Yesu anaelewa mizigo yako, mapambano yako, na vishawishi. Yupo tayari zaidi ya kukusaidia, kukuponya, kukusamehe, kukuinua, na kukuimarisha. Je! Utaruhusu upendo wake, neema, na huruma viyeyushe upinzania wo wote au tofauti yo yote unayojihisi dhidi yake leo?

Taarifa ya Sifa:

- Waadventista wengi na Wakristo wengine wanatambua kuwa tumestarehe mno na tumekuwa tukiendesha makanisa yetu kibinadamu. Tulihitaji wito wa kutuamsha ili utusaidie kuishi maisha ya imani, maombi, na miujiza kama kanisa la awali lilivyofanya katika Matendo ya Mitume. Enzi hizo waumini hawakuwa na fedha, shahada, majengo au taasisi, na bado kwa sababu ya majaribu na hata mateso na kwa uwepo na nguvu ya Roho Mtakatifu waliubadilisha ulimwengu na kuipeleka injili ulimwenguni kote kwa miaka michache tu.

MAMBO YA KUOMBEA

- Ombea makanisa kule Jamaika. Ombea washiriki wanaokabiliana na ugumu wa kifedha pamoja na wafanyakazi wa hospitali ya Andrews Memorial na wagonjwa wakati wa zahama hii.
- Ombea washiriki wa kanisa na wanafamilia wanaopambana na uraibu wa picha za ngono, pombe, sukari, sinema, muziki na vitu vingine na tabia. Waombee wapate ushindi katika Kristo.
- Ombea kanisa liitwalo *Windhoek South Church* kule Namibia ambalo kwa miaka kumi sasa limekuwa likijaribu kupata kibali cha kununua kiwanja na kujenga kanisa kwa ajili ya waumini kukusanyika.
- Ombea kiwanda cha mikate cha Kiadventista kule Granna, nchini Sweden, kiwe na uwezo wa kuwapelekea ujumbe wa injili watu wengi katika mji wao.